



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani
S.L.P 4019, DODOMA

Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222

Faksi: +255 22 2111281

Barua Pepe: info@chragg.go.tz

Tovuti: www.chragg.go.tz

Desemba 10, 2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB wakati wa maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani, Desemba 10, 2019

Leo Desemba 10, 2019 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau wa haki za binadamu ulimwenguni kote kuadhimisha miaka 71 ya Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu (*Universal Declaration for Human Rights*).

Desemba 10, 1948 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu ambalo linaainisha haki za msingi za binadamu. Azimio hili linatoa mwongozo kwa Serikali na jamii duniani kote kuhakikisha kuwa zinaheshimu, zinalinda na kukuza haki za binadamu kama zilivyoainishwa katika mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa.

Katika maadhimisho ya mwaka huu kitaifa kauli mbiu yetu inasema: ***Maadili katika utumishi wa umma ni nguzo muhimu katika kuimarisha utawala bora na haki za binadamu.***

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inatambua kuwa maadili ya viongozi, watendaji na watumishi katika utumishi wa umma ndiyo muhimili mkuu

